NORTHERN TERRITORY
Office of the
Public Guardian

Fact sheet

Kuhusu mlezi wako

Karatasi ya ukweli (Swahili)

Katika karatasi hii ya ukweli

E Kama una mlezi, ni mhimu kujua vitu wanavyovifanya. Hii karatasi ya ukweli inaeleza:

Mlezi wako ana weza kufanyaje	Maamuzi wanayoweza kukusaidia kuamua juu ya maisha yako
Mlezi wako anavyo chaguliwa	Hatua zanazochukuliwa kupata matokeo mazuri
Kitu cha kufanya kama hukubaliani na maamuzi	Vitu unavyoweza kuvifanya kama hukubali maamuzi yaliyofanywa kwako

Mlezi wako atafanya nini?

Kupata msaada wa maamuzi mhimu

Mlezi ni mtu ambaye amewekwa rasmi kukusaidia kufanya maamuzi muhimu kuhusu mambo yako kama:

- afya
- pesa
- mali
- nyumba (mahali unapoishi na watu unaoishi nao).

Unaweza kuhitaji mlezi ikiwa una shida katika kufanya maamuzi mazuri au salama katika maeneo mengine ya maisha yako. Tunaita hii kuwa na 'Kutokuwa na uwezo wa kufanya maamuzi'.

Kuwa na mlezi mmoja au zaidi

Unaweza kuwa na mlezi mmoja au zaidi kulingana na hali yako. Mahakama ya Utawala wa Kaskazini itawachagua.

Ikiwa una mlezi zaidi ya moja na hawawezi kukubaliana juu ya uamuzi wa pamoja, wanaweza kuuliza Mahakama kwa msaada.

Kuamua kitu anachoweza kukifanya mlezi wako

Mahakama itasema nini maamuzi ambayo kila mlezi anaweza kufanya na utapata nakala ya habari hii. Inaitwa utaratibu wa ulezi.

Unaweza kuwa na mlezi ambaye anakusaidia tu kusimamia fedha zako, au anayekusaidia kufanya maamuzi kuhusu mahali unapoishi na huduma yako ya afya.

Ikiwa una mpango wa kibinafsi wa mapema, hii itaendelea kukusaidia hata ikiwa una mlezi.

Kutembelea daktari au mganga wa meno

Ikiwa mlezi wako anaangalia huduma yako ya afya, watakusaidia kuamua kuhusu aina nyingi za matibabu ambazo daktari wako au daktari wa meno atashauri.

Akini kuna baadhi ya maamuzi ya afya ambayo mlezi wako hawezi kukubaliana. Mahakama pekee ndiyo inaweza kufanya maamuzi kuhusu kile tunachokiita 'huduma za afya zenye kikwazo'.

Angalia karatasi yetu ya ukweli 'Kuelewa Sheria ya Ulezi ya NT ya Watu Wazima' kwa zaidi kuhusu maamuzi ya huduma za afya zenye vikwazo.

Mlezi wako anachaguliwa namna gani?

Kuomba amri ya ulezi

Mtu mzima ambaye anayekujali wewe na kuamini kuwa unahitaji msaada katika kufanya maamuzi anaweza kuomba Mahakama amri ya.

Wanaweza kukuuliza:

- unafikiria nini kuhusu maombi
- nani unafikiria aweza kuwa mlezi wako.

© Office of the Public Guardian, 2018

Kuja kwenye maombi ya kusikia

Mahakama itaanzisha kusikia hivyo mtu anayeomba amri ya ulezi aweze kueleza kwa nini unahitaji mlezi.

Usikilizaji ni kuhusu wewe hivyo ni vizuri ikiwa unaweza kuja mwenyewe, au kuzungumza kwa video au simu, kusema nini unafikiri.

Lakini sio tatizo ikiwa hutaki kwenda kwenye kusikia, au ikiwa ungependa mtu mwingine azungumze kwa niaba yako.

Unaweza pia kuuliza mwanasheria kwa gharama yako mwenyewe ili kukuwakilisha katika kusikia, au kupata rafiki anayeaminika kuwepo. Ikiwa unafikiri huhitaji mlezi, au unataka mtu mwingine awe mlezi wako, unahitaji kusema hivyo.

Kukujulisha kilichotokea

Ikiwa mlezi anachaguliwa, Mahakama na mtu aliyechaguliwa kuwa mlezi wako watawajulisha.

Mahakama itakupa nakala ya amri ya ulezi, ambayo itakuambia nini mlezi wako anayeweza kukufanyia.

Inakuwaje kama haukubaliani?

Kubadilisha amri ya ulezi

Ikiwa huna furaha na sehemu yoyote ya utaratibu wa ulezi, unaweza kuuliza Mahakama ili kuiangalia tena.

Mahakama itaweka tarehe ya kusikiliza upya ili waweze kuamua ikiwa bado unahitaji mlezi au ikiwa amri yako inapaswa kubadilika.

Kuuliza mlezi kuhusu maamuzi

Ikiwa hukubaliana na uamuzi ambao mlezi kwa ajiri yako, unapaswa kuzungumza nao kwa nini. Unaweza kuuliza mtu mwingine kukusaidia kufanya hivyo ikiwa unahitaji.

Unaweza pia kuzungumza na Mahakama au ofisi yetu (Mtumishi wa Umma) kuhusu uamuzi. Nambari za simu ziko kwenye karatasi hii ya ukweli.

Kupitia uamuzi wa mahakama

Ikiwa hukubaliana na uamuzi ambao Mahakama imefanya, unaweza kuomba ukaguzi.

Unaweza pia kukata rufaa kwa Mahakama Kuu juu ya swali la sheria, kama inahitaji.

Sehemu ya 5 ya *Sheria ya Mahakama ya Kiraia na Utawala ya Mkoa wa Kaskazini ya 2014* (*Northern Territory Civil and Administrative Tribunal Act 2014*) kuhusu haki yako ya mapitio na rufaa.

Nyaraka muhimu

- *Sheria ya Ulezi ya NT ya Watu Wazima ya 2016* (*Guardianship of Adults Act 2016*)
- *Sheria ya Mahakama ya Kiraia na Utawala ya Mkoa wa Kaskazini ya 2014* (*Northern Territory Civil and Administrative Tribunal Act 2014*)
- *Sheria Maalumu ya Mipango Binafsi ya 2013* (*Advance Personal Planning Act 2013*)

Ofisi ya Ulezi wa Umma

kwa habari na msaada wa ulezi

1800 810 979
(8 am mpaka 4 pm siku za kazi)

public.guardian@nt.gov.au

www.publicguardian.nt.gov.au

Mahakama ya Kiraia na Utawala ya Mkoa wa Kaskazini

Kwa maamuzi ya ulezi, maombi na mabadiliko

1800 604 622
(8.45 am mpaka 4 pm siku za kazi)

agd.ntcat@nt.gov.au

www.ntcat.nt.gov.au

Ofisi ya Mahakama ya Darwin

The Met Building, CASCOM Building 5, Casuarina Village, Level 1, 13–17 Scaturchio Street, Casuarina NT 0811

PO Box 41860, Casuarina NT 0810

08 8922 7201

Ofisi ya Mahakama ya Alice Springs

Westpoint Building, 1 Stott Terrace, Alice Springs NT 0870

PO Box 1745, Alice Springs NT 0870

08 8951 5442

© Office of the Public Guardian, 2018